# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA MANISPAA MTWARA-MIKINDANI**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MTWARA**

Namba za simu

**Mkuu wa Shule:** 0754416485/0785-233324

**Makamu Mkuu wa Shule:** 0718006996

**Mwalimu wa Malezi :** 0712 214 660

Sekondari ya Wasichana Mtwara

S.L.P 164

MTWARA

Tarehe…………..

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………....................................**
**S.L.P ……………………………………....**

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI WASICHANA MTWARA ILIYOPO HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA-MIKINDANI MKOA WA MTWARA MWAKA .......**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka…………….. na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari ya Wasichana Mtwara ipo umbali wa Kilometa saba **(7)** Kusini mwa Mji wa Mtwara, Usafiri wa basi kutoka mjini Mtwara unapatikana katika kituo cha mabasi cha **MKANALEDI**, Nauli ni Shilingi 2000 kwa pikipiki na Shilingi 5000 kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe .................... hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ....................... Mwisho wa kuripoti ni tarehe ………………..

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

### 2.1 Sare za Shule

1. Mashati mawili meupe mikono mifupi yenye ukubwa wa kutosha bila kuchomoka likichomekewa AU Nusu kanzu ndefu nyeupe mbili (na isibane kwa kuonyesha umbile) na majuba meupe mawili kwa wanaovaa hijabu**.** Vinapatikana karibu na shuleni
2. Sketi mbili (2) kitambaa cha Kotoni nzito (Nyekundu) mshono wa linda box NDEFU hadi kwenye visigino vya miguu. Ili kuleta mfanano sketi zinapatikana karibu na shuleni kwa shilingi 25,000/= kwa sketi moja.
3. Magauni mawili MAREFU hadi kwenye visigino vya miguu za kushindia (Shamba Dress) rangi ya Bluu nyeusi (dark blue) kitambaa cha Kotoni nzito mshono wa Linda Boksi. Ili kuleta mfanano magauni yanapatikana karibu na shuleni kwa shilingi 35,000/= kwa gauni moja.
4. Majuba mawili (2) ya Rangi ya Bluu mpauko (light blue) (kawaida isiyo na maua) ya kujistiri baada ya muda wa vipindi (Kwa waislamu) inapatikana karibu na maeneo ya shule.
5. Viatu vyeupe (Raba za kamba) vya kufunika miguu visivyo na visigino virefu (jozi mbili).
6. Soksi nyeupe ndefu (jozi mbili).
7. Sweater (Rangi ya kijivu) kwa ajili ya kipindi kifupi cha baridi wakati wa darasani.
8. T-Shirt ya kuvaa baada ya muda wa darasani au siku maalumu na tukio maalum zitapatikana jirani na shule.
9. Track Suit moja (1) ya michezo rangi ya Kijivu. Zinapatikana karibu na shule
10. Shuka Jozi mbili rangi ya Bluu bahari. Zinapatikana karibu shule.
11. Nguo za ndani za kutosha na vifaa vya usafi (Pedi)

**Ili kuleta ufanano katika mashono na rangi kwa sare za shule na kuondoa usumbufu wa Kushona sare tofauti na maelekezo ya shule tunashauri sare uje kushona kwa mafundi walio karibu na maeneo ya shule.**

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

I. Madaftari (counter book Q3) CBG **10** Kwa Tahsusi zingine **8**
II. Godoro( ft 2.5 x 6)
III. Chandarua (Rangi nyeupe)
IV. Vyombo vya chakula (Sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
V. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.
VI. Raba za michezo.
VII. Sanduku imara la kutunzia vifaa vyake (Tranka).
VIII. Tochi ya kumsaidia wakati umeme unapokatika.
IX. Vitabu vya masomo ya Tahasusi husika. ( Unashauliwa kuja kununua kwa wauzaji waliopo shuleni ili kupata kitabu sahihi)
X. Dissecting kit kwa wanafunzi wa CBG.
XI. Scientific Calculator kwa wanafunzi wa EGM, HGE na CBG.
XII. Rimu 2 (chapa ya **DOUBLE A,** tofauti na hiyo haitapokelewa )
XIII. Stapler 1 (**kangaro DS-45NR**)
XIV. Staples (pini za stapler) box 1 (**24/6-1M kampuni ya kangaro box jekundu**)
XV. Graph pad 2 kwa wanafunzi wa **HGE, EGM** na **CBG**
XVI. Vifaa vya usafi wa mazingira
    a. Kwanja 1
    b. jembe lenye mpini 1

c. Dawa ya kusafishia chooni Lita Tano. (**Tarmol,** tofauti na hiyo haitapokelewa) .
d. Fagio laini (Soft broom) moja (1)
e. Fagio gumu (Hard broom) moja.
f. Squeezer 1
g. Toilet brush 1
h. Fagio ya nje (chelewa) moja (1).

XVII. Kadi ya bima ya afya na kama hautakuwa nayo utatakiwa kuwa kiasi cha shilingi elfu hamsini na mia nne(50,400) kama gharama za kukatia bima ya afya.

**NB: Ili kuepusha usumbufu wa mizigo njiani kwa anayehitaji huduma/mahitaji tajwa hapo juu yanapatikana kwenye maduka yaliyopo nje kidogo ya eneo la shule, kwa hiyo ni vyema ukajua gharama ya vitu hivyo**.

| S/N | MAHITAJI | IDADI | BEI KWA MOJA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shuka za bluu | 2 | 10,000/= | 20,000/= |
| 2 | Sketi ya shule | 2 | 25,000/= | 50,000/= |
| 3 | Gauni la kushindia | 2 | 35,000/= | 70,000/= |
| 4 | T-shirt ya shule | 1 | 15,000/= | 15,000/= |
| 5 | Majuba | 4 | 15,000/= | 60,000/= |
| 6 | Track suit | 1 | 25,000/= | 25,000/= |
| 7 | Sweta | 1 | 15,000/= | 15,000/= |
| 8 | Sabuni ya kusafishia chooni(Tarmol) | 1 | 13,000/= | 13,000/= |
| 9 | Toilet brush | 1 | 3,000/= | 3,000/= |
| 10 | Counter book Q3 | | 3,000/= | |
| 11 | Dissecting kit(kwa wanafunzi wa CBG) | 1 | 35,000/= | 35,000/= |
| 12 | Scientific calculator | 1 | 45,000/= | 45,000/= |
| 13 | Jembe na mpini | 1 | 9,000/= | 9,000/= |
| 14 | Reki | 1 | 7,000/= | 7,000/= |
| 15 | Fyekeo | 1 | 5,000/= | 5,000/= |
| 16 | Soft bloom | 1 | 4,000/= | |
| 17 | hard bloom | 1 | 4,000/= | |
| 18 | squeezer | 1 | 4,000/= | |

## 2.3 Michango mbalimbali

Michango ifuatavyo anapaswa kuja nayo wakati wa kuripoti

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Michango inatakiwa ilipwe kupitia Benki ya NMB katika ACCOUNT **Na**. **70601200072** ya Mtwara Girls Secondary School. Jina la akaunti **Mtwara Girls Secondary School.** Pia uje na risiti halisi (Original) ya benki (Bank Pay In Slip) iliyoandikwa jina la mwanafunzi.

## 3.0.Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi anatakiwa kuja na nguo nyepesi za kulalia na si zile nzito**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi. Hata ivyo kwa shule yetu mwanafunzi haruhusiwi kusuka
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Vifuatavyo viambatanishwe na fomu hii**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**TAARIFA BINAFSI KUHUSU MWANAFUNZI**
(Form hii ijazwe na irudishwe shuleni)

1. Jina la mwanafunzi ........................................................................... Kidato cha **V** Mchepuo ................

2. Kabila la mwanafunzi ..............................................................................

3. Dini ya mwanafunzi; ...........................................................................................................................

3. (a) Tarehe ya kuzaliwa; .......................................................................................................................

(b) Wilaya alikozaliwa mwanafunzi; .................................................................................................

(c) Mkoa; ..................................................................................................

4. Jina kamili la baba; ..................................................................................

Makazi: **Kijiji/Mtaa** ……………………….. **Wilaya** ……………………. **Mkoa** ……………………….

Namba ya simu ....................................................... Kazi yake: ..............................................................

5. Jina kamili la mama; ..................................................................................

Makazi: **Kijiji/Mtaa** ……………………….. **Wilaya** ……………………. **Mkoa** ……………………….

Namba ya simu ....................................................... Kazi yake: ..............................................................

6. Jina kamili la mlezi anayemhudumia mwanafunzi ikiwemo kumpatia mahitaji yake muhimu;
...................................................................................................................

Uhusiano wa mwanafunzi na mlezi; ..........................................................

Makazi: **Kijiji/Mtaa** ……………………….. **Wilaya** ……………………. **Mkoa** ……………………….

Namba ya simu ....................................................... Kazi yake: ..............................................................

7. Baba na mama wanaishi pamoja / wametengana (kata isiyohusika)

8. Uwepo wa wazazi: Baba - YUPO/HAYUPO kama amefariki lini .................................................
Mama - YUPO/HAYUPO kama amefariki lini .................................................

9. Majina na picha za watu wasiozidi wanne watakaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa dharula au wito maalumu;-

| **PICHA** | **PICHA** | **PICHA** | **PICHA** |
|---|---|---|---|
| JINA | JINA | JINA | JINA |
| SIMU | SIMU | SIMU | SIMU |
| UHUSIANO | UHUSIANO | UHUSIANO | UHUSIANO |

**UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI**

**Mimi** .................................................................... ambaye ni mzazi wa ..................................................

aliyetoka shule ya .....................................................Wilayani ..................................Mkoa wa................

nimesoma na nimeyaelewa maagizo ya kujiunga na shule hii na ninaahidi kuwa nitajitahidi kumpatia mahitaji muhimu binti yangu aliyetajwa hapo juu hadi atakapomaliza ELIMU YA SEKONDARI.

Sahihi .................................................................. Tarehe .......................................................................

**UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI**

**Mimi** ......................................................................................... wa kidato cha ....................................

Nimesoma na kuzielewa sheria za shule, na naahidi kuzitii na kutimiza taratibu zote zilizowekwa.

Sahihi .................................................................. Tarehe .................................................................

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

Saini ya Mkuu wa Shule ........................

Jina la Mkuu wa Shule: ..................

Mhuri wa Mkuu wa Shule ..........................

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- Mkuu wa shule 0754416485 /0785233324
- Makamu Mkuu wa Shule 0718006996
- Mwandamizi Taaluma 0653652509
- Mwandamizi Malezi 0654966801
- Muuguzi wa shule 0683146813/0719141862

## MTWARA - MIKINDANI MUNICIPAL COUNCIL

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

THE HEADMISTRESS,
MTWARA GIRLS SEC/SCHOOL,
P. O. BOX 164,
**MTWARA.**

DATE: ..................................

TO:
The Medical Officer
..................................................
..................................................
…………………………………

**RE: NAME OF STUDENT ..........................................................................................................**

Please examine the above as to his/her physical and mental fitness for full time course of Secondary Education at Mtwara Girls Secondary School.

1. Eye sight ..............................................................................................................................
2. Hearing ..............................................................................................................................
3. Speech ..............................................................................................................................
4. Venereal Diseases ..............................................................................................................
5. Neurosis ..............................................................................................................................
6. Pregnancy ..........................................................................................................................
7. VDRL ………………………………………………………………………………………
8. TB ………………………………………………………………………………………….
9. Asthma……………………………………………………………………………………..

Doctor's Remarks ..................................................................................................................
.....................................................................................................................................................
.....................................................................................................................................................

Doctor's Advice ......................................................................................................................
.....................................................................................................................................................
.....................................................................................................................................................

Doctor's Name ........................................................................................................................
Signature ............................................. Rubber Stamp ……………………………………….
Date .........................................................................................................................................